

NGONJERA NA MTAZAMO MPYA WA MALEZI YA WATOTO NA VIJANA

Shadidu A. Ndossa

Ikisiri

Malezi ya watoto na vijana kwa jumla ni ada muhimu katika ustawii wa jamii yoyote inayohitaji kupiga hatua za kimaendeleo. Isivyo bahati, jamii imeshughulishwa mno masuala mengine ya kimaisha, na kuwaacha watoto na vijana wajilee wenyewe. Wakati haya yakitokea, waandishi wawili—Ramadhan Nyembe na Abdallah Seif—wanajitokeza kuikumbusha jamii kuhusu ulezi wa watoto na familia kupitia ngonjera. Makala hii inachambua mchango wa wasanii hawa wa ngonjera katika kuirejesha jamii katika mstari wa malezi kupitia tungo zao mbili, Ngonjera Elimishi Na.1 na Ngojera: Nasaha na Uzalendo. Uchambuzi wa matini umetumika kama njia ya kupata taarifa mbalimbali za kitabuni. Aidha, nadharia ya uhalisia imetuongoza katika uchambuzi na uwasilishaji wa taarifa mbalimbali za kitabuni. Hii ni kusema kuwa, mambo mengi yaliyozungumzwa na waandishi ni mwangwi wa maisha halisi yanayojitokeza katika jamii. Ili kufikia lengo la makala hii, mwandishi ameshughulikia ngonjera zinazohusiana na malezi ya watoto na vijana tu. Kwa jumla, wasanii wameweza kufikisha ujumbe muhimu kwa jamii. Wamezungumzia mambo muhimu kama vile umuhimu wa elimu kwa watoto, madhara ya pombe na dawa za kulevyta, imani za kishirikina na heshima kwa wakubwa.

Utangulizi

Kwa miaka mingi, ngonjera imetumika sana katika uga wa siasa kuhamasisha uzalendo na kufanya kazi kwa bidii. Mwishoni mwa miaka ya 60 na katika miaka ya 70, ngonjera zilitumika kwa nguvu kubwa katika kuelimisha wananchi kuhusu siasa ya ujamaa na kujitegemea (Mulokozi na Sengo, 2005). Mathias Mnyampala alikuwa mshika bango mkuu wa utanzu huu kiasi cha kuufanya kufahamika na kupenya katika majukwaa ya kisiasa na kijamii. Ndiyo maana Sengo na Mulokozi pamoja na waandishi wengi wa Kiswahili wanamuona Mnyampala kama mtu muhimu aliyeihuisha sanaa hii ya jadi (Massamba, 1983). Katika miaka hiyo ya mwanzo, ilikuwa kama dhambi kwa vikao na mikutano ya siasa kufanyika bila kutoa nafasi kwa utanzu huu. Wanafunzi katika shule walikuwa wakishindana na kuonesha umahiri wa kuhifadhi beti mbambali za ngonjera.

Kwa upande mwingine, mgogoro wa ushairi wa miaka ya 70 na maendeleo makubwa ya kiteknolojia katika miaka ya 1990 na 2000 yameibua mitindo mipy ya sanaa na fasihi kwa jumla (Ponera, 2014 na Abdallah, 2018). Hali hii imepunguza kwa kiasi kikubwa hadhira na matumizi ya ngonjera katika miktadha

mbalimbali ya kijamii. Kwa mfano, shughuli mbalimbali za kitaaluma na kisiasa (kama mahafali, vikao vya chama na mikutano ya kampeni) ambazo huko nyuma zilitoa nafasi kubwa kwa ngonjera, siku hizi zimetawaliwa na nyimbo za wasanii wa kizazi kipy. Hatimaye, ngonjera zimepoteza mvuto na hazisikiki. Katika hali hiyo ya ufufumavu wa ngonjera, waandishi—*Ramadhan Nyembe na Abdallah Seif*—kutoka Dodoma wameamua kuchapisha vitabu vya ngonjera kama sehemu ya kuenzi sanaa hii ambayo ilisukumwa kwa kiasi na mwana-Dodoma mwenzao, Mathias Mnyampala. Kwa namna ya kipekee, kazi hizi zimefanya ukengeushi wa kimaudhui kwa kutilia mkazo masuala ya kijamii, kinyume na huko nyuma ambapo ngonjera zilijikita zaidi katika maudhui ya kisiasa. Kazi zote mbili zimeshabihiana kwa kiasi kikubwa katika kuongelea suala la malezi ya watoto na vijana. Hivyo basi, makala hii inaangazia kwa kina mchango wa kazi hizi mbili za ngonjera katika suala la malezi ya vijana na watoto.

Mjadala wa makala hii umejiegemeza katika vitabu vitabu viwili, *Ngonjera Elimishi Na.1 na Ngonjera: Nasaha na Uzalendo*. Uteuzi wa kazi hizi umesukumwa na mambo makuu mawili yafuatayo: Jambo la kwanza ni muhula au kipindi cha uchapishaji. Kazi zote mbili zimechapishwa mwaka 2018. Imeelezwa hapo juu kuwa miaka ya 1960 na 70 ndiyo kipindi au muhula maarufu kwa ngonjera. Ni muda mrefu umepita bila kuchapishwa kwa vitabu vya ngonjera tangu kipindi kile. Hivyo, muda uliochapishwa kazi hizi umemsukuma mwandishi wa makala hii kujadili maudhui ya kazi hizi. Jambo la pili ni maudhui yake. Maudhui ya kazi hizi yametuama katika kuelezea suala la malezi ya watoto na vijana. Kama ilivyodokezwa huko nyuma, huu ni mwondoko mgeni wa kimaudhui katika ngonjera. Hii ni kwa kuwa ilishazoelekea kuwa ngonjera hujiegemeza sana katika mambo ya kisiasa.

Yafuatayo ni maeleo mafupi ya diwani hizo teule zinazoelezwa katika makala hii:

Ngonjera Elimishi Na.1 ni kitabu kilichoandikwa na Abdallah A. Seif (ambaye hutumia lakabu ya ‘Mkonikoni Ngome Imara’). Mwandishi ni mwenyeji na mkazi wa Dodoma. Kitabu kimechapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2018. Kitabu kina jumla ya ngonjera 13 ambazo zimeandikwa kwa muundo wa visa²³ vinavyoolezea maudhui mbalimbali. Pia, ili kuongeza uelewa na urahisi kwa msomaji, kitabu kimejumuisha sura maalumu kwa ajili ya msamiati na maneno magumu. Kwa jumla, ngonjera kumi na moja (11) kati ya kumi na tatu (13) zinazungumzia masuala ya kijamii kama vile hatari ya madawa ya kulevy,

²³ Mwandishi wa kitabu ametumia mfumo wa visa au hadithi ambapo wahusika wawili au zaidi hushindana/kubishana kuhusu jambo fulani na baadaye hufikia hitimisho kwa pande mbili kuafikiana. Mbali ya mabishano ya pande mbili, mwandishi pia amemtumia msimulizi katika baadhi ya visa vyake.

umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike, na hatari ya imani za kishirikina. Pia, ngonjera mbili (2) zinazungumzia masuala ya siasa, hasa elimu na uwajibikaji wa viongozi kwa wananchi waliowachagua. Mwandishi ametumia lugha fasaha na inayoeleweka kwa wasomaji. Ametumia lugha ya kisanaa inayojumuisha methali, misemo, misimu na uchanganyaji ndimi. Mwandishi ametumia pia wahusika ambao wanavisukuma mbele visa husika kwa kupitia majibizano na mabishano yao. Mionganoni mwa wahusika hao ni mhusika msimulizi, hasa katika kuelezea mapito mbalimbali na kuhitimisha visa vyake.

Kwa upande wa *Ngonjera: Nasaha na Uzalendo*, mwandishi wake ni Ramadhani M. Nyembe. Mwandishi ni mkazi na mwenyeji wa Dodoma. Mwandishi huyu, amerithi na kuendeleza kipaji hiki kutoka kwa marehemu baba yake ambaye alikuwa ni mwandishi maarufu wa Dodoma, Sheikh Mohamed Ally Nyembe²⁴. Kama ilivyo kwa kitabu cha awali, kitabu hiki kimechapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2018. Pia, mwandishi ametunga ngonjera zake katika mfumo wa visa. Hata hivyo, visa vyake sio vya moja kwa moja kama vilivyojitezea katika kitabu teule cha awali. Kitabu kina jumla ya ngonjera tano zilizo katika sura sita. Mwandishi ametuamisha maudhui yake katika masuala ya kijamii katika ngonjera nne kati ya tano. Ngonjera moja inaelezea masuala ya kisiasa, hasa umuhimu wa uzalendo kwa wananchi. Kwa upande wa lugha, mwandishi amejitahidi kutumia lugha fasaha na inayoeleweka kwa urahisi kwa msomaji. Pia, mwandishi ametenga sura maalumu ambayo inatoa ufanuzi wa msamati na maneno magumu yaliyotumika katika kitabu. Aidha, mwandishi ametumia lugha ya kisanaa kama methali, nahau, misemo na lugha ya picha.

Nasaha za Waandishi kuhusu Malezi ya Watoto na Vijana

Kama ilivyozungumzwa huko nyuma, waandishi wote wawili wametilia mkazo saula la malezi ya watoto na vijana kwa namna ya pekee na inayoshabihiana sana. Wote wanaamini kuwa malezi ya watoto na vijana ni ngazi muhimu ya kuchochea maendeleo ya taifa la Tanzania kama itakavyojadiliwa hapa chini.

Malezi ya Watoto

Waandishi wote wamezungumzia umuhimu wa wazazi kuwapa malezi bora watoto wao. Wanaona kuwa suala la malezi ni jukumu la mama, baba na ndugu wa karibu. Aidha, wanakemea tabia ya wazazi kuwaacha watoto kuzurura mitaani, kwani tabia

²⁴ Sheikh Mohamed Ally Nyembe (1932 – 1999) ni mionganoni mwa washairi maarufu wa Dodoma, Tanzania. Kishairi, alijulikana kwa jina la Akhery. Wakati wa uhai wake alitunga mashairi mengi ambayo hakubahatika kuyachapisha katika vitabu. Baadhi ya mashairi yake yameanza kuchapishwa mwaka 2019; yamo katika diwani ya *Adili za Nyembe 1* (Ndossa, A., Hassan, H.R., & Ponera, A.S. [Wah.]).

hiyo hupanda mbegu mbaya kwa watoto na; hivyo, kuchangia kuperomosha maadili ya jamii. Kwa mfano, katika “Nasaha za Mke” mwandishi anasema maneno yafuatayo:

Mke: Haki ya wetu watoto, kweli waitupa mbali,
 Malezi yao ni ndoto, na huo ndio ukweli,
 Hulitilii uzito, huduma ya kila hali,
 Kweli waitupa mbali, haki ya watoto wetu

Ngonjera: Nasaha na Uzalendo (Ubeti wa 13, Uk. 54).

Katika ubeti huu inaonekana wazi namna ambavyo mke anavyoumia kutokana na malezi duni yanatolewa kwa watoto (muhimu kutaja hapa kuwa aliyekuwa analezwaa hapa ni mume ambaye kutokana na ulevi alishindwa kabisa kuitunza familia na, hivyo, kushindwa kutoa malezi na mahitaji mengine muhimu kwa watoto wake). Katika sehemu hii mwanamke alikuwa anamkumbusha mume wake kuwa suala la kuwatunza watoto na familia ni jukumu la wazazi wote; ndiyo maana akawa anapata tabu kuona baba hajihusishi na suala la malezi ya watoto kama anavyosema tena:

Mke: Tumia wako wasaa, kuitunza familia,
 Na ipate manufaa, kwa malezi na tabia,
 Tena usije jikwaa, moyoni utie nia,
 Kuitunza familia, timiza wako wasaa.

Ngonjera: Nasaha na Uzalendo (Ubeti wa 13, Uk. 54).

Mke hapa anaendelea kusisitiza umuhimu wa mume kutumia muda na rasilimali zake zote katika ulezi wa watoto na familia kwa jumla. Mke anaona kuwa suala la mafanikio katika familia huenda sambamba na suala la malezi bora. Anajaribu kumsihi mume wake kuongeza juhudii katika malezi ya familia; na, atambue kuwa hilo ni jukumu lake na sio la mtu mwingine.

Kwa upande wake, mtunzi wa *Ngonjera Elimishi Na. I* anazungumzia umuhimu wa malezi ya watoto kupitia ngonjera ya “Mwanamke Aliyechwa kwa Kuzaa Albino”. Mwandishi anaonesha namna wazazi, hasa wa kiume, wanavyokwepa majukumu ya kulea watoto kwa kisingizio cha mwanamke kuzaa watoto walemavu. Katika hili, mwandishi anasema maneno yafuatayo:

Kalunde: Mimi ulinisimanga, ulisema nakuboa,
 Watoto ukawatenga, badala kuwaongoa,
 Kwa ndweo ultunanga, na kashifa ukifyoa,
 Maneno ilitongoa, ya kedi na simangizi.

Ngonjera Elimishi Na. I (Ubeti wa 57, Uk.63).

Katika ubeti huu, mwandishi anabainisha malalamiko ya mke juu ya kutengwa kwake baada ya kuzaa watoto walemavu. Aidha, mwandishi anaonesha kuwa mzazi wa kiume (baba) aligoma kutoa matunzo ya watoto, hivyo mzigo wote wa malezi kumuangukia mama. Jambo hili la wazazi kushindwa kutoa malezi kwa watoto linajitokeza sana katika jamii zetu. Jambo hili sio zuri kwa kuwa linawanyima watoto haki zao ya msingi kama vile elimu na afya (Chikaka, 2017).

Heshima kwa Wazazi na Wakubwa

Waandishi wote wawili wamezungumzia suala la watoto kuwaheshimu wazazi na watu wazima. Wanaona kuwa suala la heshima kwa wakubwa ni la kidini na la kitamaduni. Wanahuisha heshima kwa wazazi na baraka za Mungu pamoja na daraja la mafanikio mema kwa jamii nzima. Waandishi wanakemea tabia ya watoto kuwadharau na kuwakejeli wazazi kama mwandishi wa *Ngonjera Elimishi Na.1* anavyosema kupitia ngonjera ya “Heshima na Utii kwa Wazazi”:

Mponda: Wazazi wako kwa kweli, walineni na kuguna,
 Walilaumu vikali, tabia yako kijana,
 Walisema huwajali, adabu kabisa huna,
 Utii jambo la maana, heshimu wazazi wako.

Kibwana: Baba na mama hupenda, kunituma kila kona,
 Niende vuna matunda, mara nikasage dona,
 Mimi mtu siyo punda, huwaambia hapana,
 Kutumwatumwa naona, kwanipotezea muda.

Ngonjera Elimishi Na.1 (Ubeti wa 4 & 7, Uk. 12).

Kupitia majibizano ya Mponda na rafiki yake, Kibwana, mwandishi anajaribu kuonesha namna watoto wanavyokosa utii mbele ya wazazi wao. Mwandishi anakemea kuwa, jambo hili halifai kwa kuwa ni jukumu la watoto kuwaheshimu wazazi na kufuata maelekezo wanayopewa. Aidha, mwandishi anabainisha malalamiko ya wazazi kuwa anachofanya Kibwana ni makosa na anapaswa kujirekebisha. Mwandishi anaona watoto wanao wajibu wa kuwalea wazazi wao kama anavyosisitiza mwishoni mwa ngonjera kwa maneno yafuatayo:

Mtangazaji: Mtunzi natoa wito, wazazi kutowakana,
 Uzazi ni jambo zito, hili ubishi halina,
 Pia kulea mtoto, ni tabu yajulikana,
 Tukijua hilo tena, hatutobeza wazazi.

Ngonjera Elimishi Na.1 (Ubeti wa 23, Uk.12).

Katika ubeti huu mwandishi anasema wazi kuwa suala la kuzaa na kulea ni zito. Hii ni kusema kuwa wazazi hupitia mashaka makubwa katika kuwalea watoto. Hivyo, ni jukumu la watoto nao kulipa fadhila kwa kuwaheshimu na kuwatunza wazazi wao, hasa wanapofikia umri wa uzeeni. Aidha, mwandishi anakemea vikali tabia ya watoto kufuata tabia za marafiki ambazo zinalenga kuwadharau wazazi wao. Mwandishi anaona kuwa wazazi wanao wajibu wa kuwakataza watoto wao kuungana na marafiki wabaya ambao wataharibu tabia nzuri za watoto.

Nyembe (khj) amezungumzia umuhimu wa vijana kuwaheshimu watu waliowazidi umri. Mwandishi amesimama katika mapokeo ya Kiafrika ambapo watoto wanao wajibu wa kuwaheshimu watu waliowazidi umri, iwe wanawafahamu au laa. Mwandishi ametumia malumbano baina ya Mzee na Kijana kubainisha namna ambavyo vijana wanatakiwa kuongea na watu waliowazidi umri. Kupitia ngonjera hii, mwandishi anawaeleza vijana kuwa, wanaweza kuwasilisha hoja zao na kupinga hoja za watu wengine (hata kama wamewazidi umri) kwa kutumia hekima na busara kama anavyosema katika beti zifuatazo:

Mzee: Kijana una busara, amekufundisha nani?
 Umesema jambo bora, kunigusa akilini,
 Haukutaka kuzira, kujua kuna thamani,
 Au kuwa na busara.

Mzee: Kweli ni yako dhamira, kujua mambo undani,
 Hukukunja yako sura, nimekuona usoni,
 Ijapo nimekukera, kwa ukali naamini
 Ni kweli upo imara.

Ngonjera: Nasaha na Uzalendo (Ubei wa 22-23, Uk.,34).

Katika beti zote mbili mwandishi anadokeza vijana wanavyotakiwa kuongea na watu wazima. Mwandishi anaonesha kuwa, katika dunia ya leo vijana na wazee wanaweza kuketi pamoja na kujadili mambo mbalimbali yanayohusu ustawi wa jamii. Muhimu zaidi mwandishi anabainisha kuwa, ili mijadala hii ya vijana na wazee iwe na tija, vijana wanapaswa kuwa na busara na kutumia lugha nzuri pindi wanapoamiliiana na wazee au watu wazima. Aidha, mwandishi anasisitiza kuwa, ni muhimu kutojibu mapigo hasa inapotokea kupishana baina ya vijana wa wazee. Mwishoni, mwandishi anawahimiza vijana kutoonesha kukasirika kwa kunkunja sura pale wanapoongea na watu waliowazidi umri, kwani tabia hiyo ni mbaya na inakera. Ni wazi kuwa tabia ya kuwaheshimu wazazi na watu wakubwa ni katika adili muhimu ambayo daima imekuwa ikifumbatwa katika hadithi za watoto (Madumulla, 2001; Senyamanza, 2013; Bakize, 2014; Lyimo, 2014).

Kutunza Mila na Utamaduni na Kupinga Mila Potofu

Waandishi wamezungumzia pia umuhimu wa kuwafunza watoto na vijana mila na desturi mbalimbali zinazofaa, sambamba na kupinga mila zote potofu zisizofaa. Waandishi wote wanaamini kuwa samaki anapaswa kukunjwa angali mbichi kwa kuwafunza watoto mila na desturi zao wangali wakiwa wadogo. Aidha, waandishi wote wanaonekana kukubaliana kuwa, zipo mila potofu ambazo watoto na vijana wanapaswa kufunzwa kuwa hazifai na hazisaiddii jamii yetu kupiga hatua za kimaendeleo. Kwa mfano, mwandishi wa *Ngonjera Elimishi Na.1* amekemea suala la ushirikina na kuionya jamii kuwa njia hiyo ni ya giza na haifai kuwaonesha watoto. Akizungumzia kuhusu hatari ya ushirikina, mwandishi anasema:

Mzee Matonya: Muda ningeupoteza, kwa wagangamizunguko,
 Huku maradhi yakaza, na kuzidi mfumuko,
 Mwisho tungewapoteza, tungeishia maziko,
 Ni kweli wadogo zako, hawakuwa wamerogwa.

Mzee Matonya: Mganga aliyonena, jirani wana vituko,
 Mnaweza kukosana, na majirani wenzako,
 Tungeweza kuuana, kumbe ukweli hauko,
 Ni kweli wadogo zako, hawakuwa wamerogwa.

Ngonjera Elimishi Na.1 (Ubeti wa 20 & 22, Uk.11).

Katika beti zote mbili mwandishi anaonesha hatari ya watu kuamini tiba za kishirikina. Mwandishi anabainisha kuwa mambo ya kupiga ramli huleta uchonganishi katika jamii na kuzua mitafaruku isiyo na tija. Aidha, mwandishi anaonesha kuwa tiba za waganga mara nyingi huweza kusabibisha hatari kwa mgonjwa pale ambapo mgonjwa atajiegemeza zaidi huko na kushindwa kupata tiba stahiki kutoka hospitalini. Mwandishi anatumia ushuhuda wa Mzee Matonya kuonesha hali halisi ilivyo katika jamii ambapo waganga wanaaminiwa sana kiasi cha kuwafanya watu kudharau huduma rasmi za afya. Aidha, anaonesha hali ilivyo katika jamii ambapo waganga hutumika kuwafitinisha watu na kuzua sokomoko zisizo na msingi. Anaona kuwa, imani za kishirikina zinazorotesha maendeleo katika jamii, na ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo, hasa katika maeneo ya vijijini.

Kwa upande wa *Ngonjera: Nasaha na Uzalendo*, mwandishi anazungumzia umuhimu wa kuwafunza vijana kupenda kudumisha mila za Mwaafrika. Muhimu zaidi, anazungumzia umuhimu wa kuwafunza watoto na vijana tabia ya kupenda vitu vyakula vyakula vya Kiafrika. Anatumia mabishano baina ya Mzee na Kijana kuonesha namna vijana wanavyodharau vyakula vyakula vya asili huku “wakipupia” vyakula vinavyotoka nje. Anasema:

Mzee: Nyinyi mnataka keki, na maziwa ya kuoza,
Maboga hamyataki, sisi yaliyotukuza,
Mmelewa ushabiki, na kukosa muangaza,
Mnaona ndio haki.

Ngonjera: Nasaha na Uzalendo (Ubei wa 22-23, Uk. 34).

Hapa, mwandishi anapigia chapuo vijana kupenda vyakula vya asili. Makala hii inaamini kuwa, katika ngonjera hii, chakula kimetumika kuwakilisha mila, tamaduni na desturi mbalimbali za Kiafrika. Mwandishi anaona kuwa vijana wamechotwa na usasa unaosukumwa na utandawazi kiasi cha kudharau asili yao. Zaidi, anaonesha hatari inayowakabili vijana kwa kula vyakula visivyo vya asili kama vile kupata magonjwa ya kisukari, presha na unene usio wa kawaida. Kwa jumla, mwandishi anaona kuwa jamii ya sasa inadharau sana mila na desturi za Kiafrika, jambo ambalo sio sawa kwa kuwa linatishia uhai wa Mwfrika na utamaduni wake (Senkoro 2011; Mulokozi 2017; Mlaga 2017).

Umuhimu wa Elimu kwa Watoto

Waandishi wa ngonjera wamezungumzia pia umuhimu wa kuwapa watoto fursa ya kusoma. Wanapinga tabia ya wazazi na walezi kuwatumi kisha watoto na kuwanyima haki yao ya kusoma na kuelimika. Wamepigia mfano wataalamu mbalimbali ambao wazazi wao waliwapa fursa ya kusoma na, baadaye, wamekuwa msaada mkubwa kwa wazazi na jamii kwa jumla. Kupitia ngonjera ya “Elimu ni Haki Yangu”, mwandishi Seif anabainisha kilio cha watoto kwa maneno yafuatayo:

Mtoto: Elimu ni haki yangu, baba nataka kusoma,
Hili ndilo ombi langu, nakuomba kwa heshima,
Nende shule na wenzangu, asubuhi na mapema,
Baba nataka kusoma, elimu ni haki yangu.

Baba: Wasumbukaje na shule, huko nini utachuma?
Nyumbani vitu vi tele, wapata zote huduma,
Kuna nini shule kule, kizuri chenye neema?
Utafuga na kulima, na mke nitakuza.

Ngonjera Elimishi Na.1 (Ubei wa 1-2, Uk. 1).

Kupitia beti hizi mbili, mwandishi anapaza sauti ya mtoto anayelalamika kwa kunyimwa fursa ya kupata elimu. Mwandishi anapinga fikra za wazazi wanaona kuwa elimu haina umuhimu. Kama tulivyosema, mwandishi anasisitiza kuwa elimu ni haki ya mtoto. Aidha, mwandishi anakemea tabia za wazazi kuwageuza watoto kuwa wafanyakazi kwa kuwachungisha mifugo au kuwafanya vibarua katika mashamba. Mwandishi anayasema haya kwa kuwa imekuwa ni kilio kikubwa, hasa

kwa maeneo ya vijijini ambapo baadhi ya watoto hunyimwa fursa ya kusoma. Baadhi ya wazazi na walezi huwatumia watoto hawa katika kazi mbalimbali za uzalishaji mali kama vile kuchunga mifugo, kuchimba madini na kilimo (Chikaka, 2017).

Vilevile, mwandishi Seif amezungumzia kwa undani umuhimu wa jamii kumpa mtoto wa kike fursa ya kusoma. Mwandishi anaamini kuwa, jamii yoyote ile haiwezi kupiga hatua kama itamnyima fursa mtoto wa kike kupata elimu. Pia, anaona kuwa kitendo cha kumnyima fursa ya kusoma mtoto wa kike ni kinyume cha sheria na kinaandaa mazingira ya kumfanya kuwa tegemezi. Kwa jumla, anaona kuwa kumnyima mtoto wa kike fursa ya kusoma ni jambo lililopitwa na wakati kama anavyosema katika ubeti ufuatao:

William: Elimu kumpatia, mwanamke si tatizi,
 Wapo wengi Tanzania, wanawake viongozi,
 Wengine mainjinia, baba fanya uchunguzi,
 Ni lazima sasa Rozi, akaandikishwe shule.

Ngonjera Elimishi Na.1 (Ubeti wa 16, Uk. 6).

Baba: Maneno yenu hekima, mazito siyageuzi,
 Nimeyaelewa vyema, wala muda sipotezi,
 Rozi ataenda hima, masomoni simkwazi,
 Ni lazima sasa Rozi, akaandikishwe shule.

Ngonjera Elimishi Na.1 (Ubeti wa 19, Uk.6).

Beti hizi zinaonesha umuhimu wa mtoto wa kike kupata elimu kama walivyo watoto wengine. Kupitia mhusika William, mwandishi anamuelimisha Baba hatari ya kumnyima Rozi fursa ya kusoma. William anafafanua kuwa, hivi sasa Tanzania wapo viongozi wanawake (ambao bila shaka wamepata fursa ya kusoma ndio maana wakachaguliwa kuwa viongozi) na watalamu wengine mbalimbali kama wahandisi na madaktari. Mwisho, mwandishi anatumia sauti ya mzazi kupiga mbiu kwa jamii nzima kuwa zama zimebadilika; mtoto wa kike naye anapaswa kwenda shule ili ataalamike na kuelimika sawa na mtoto wa kiume.

Haki za Watoto Walemvu

Mwandishi anaeleza madhila mbalimbali yanayowakabili watoto walemvu. Anaona kuwa wazazi, hasa wa kiume, wamekuwa wakiwakanwa watoto wao pale wanapobaini kuwa ni walemvu na kuwaachia wanawake mzigo mkubwa wa malezi. Jambo hili, kwa mujibu wa mwandishi, halifai kutokana na ukweli kuwa linawanyima watoto haki zao za msingi kama anavyobainisha kwa maneno yafuatayo:

Mume: Mke wangu ni tatizo, mno ninakushangaa
Kuzaa mfululizo, albino ni balaa,
Hicho ni kielelezo, cha jinsi usivyofaa,
Hufai kwango kukaa, wewe na watoto wako

Mume: Nyumbani kwango ondoka, tena bila kukawia,
Ni uzazi wa mashaka, huu uliojizalia,
Siwezi kuwa shirika, na mtu mwenye udhia,
Ondoka nakuambia, ondoka urudi kwenu.

Ngonjera Elimishi Na.1 (Ubeti wa 1-2, uk. 55).

Katika beti hizi mbili, mwandishi anabainisha namna baadhi ya wazazi walivyo na mtazamo hasi kuhusu watoto walemavu. Mwandishi anamtumia mume kueleza hali halisi ilivyo katika miji, mitaa na vijiji vyetu ambapo watoto walemavu wanaonekana kama mkosi. Zaidi, katika hali hii mume hujiweka mbali kama vile watoto waliozaliwa sio damu yake, na mzigo wote wa lama hutwishwa mwanamke. Mwandishi anaamini kuwa watoto walemavu sio mkosi bali wamezaliwa hivyo kutoka na mipango ya Mungu. Mwishoni kabisa mwa ngonjeara hii, mwandishi anayatumia mafanikio ya watoto wawili albino (Maziku na Mabula) amba baba yao aliwakataa kuudhihirishia umma kuwa albino ni watu wa kawaida. Mwandishi anaamini kuwa watoto walemavu wanaweza kupata mafanikio makubwa kuliko hata watoto wa kawaida kama anavyobainisha kwa kusema.

Mtangazaji: Ulemavu wa ngozi yao, haukuwazuwililia,
Kutimiza ndoto zao, malengo kuyafikia,
Walijiamini wao, ni watu wametimia,
Hivyo walikazania, kusoma na kujituma.

Mtangazaji: Mmoja mwalimu shule, mwengine mfamasia
Miradi ikiwa tele, waliojianzishia,
Ikafanya wawe mbele, mavuno kujichumia,
Nyota ikawawakia, maisha yenye faraja.

Ngonjera Elimishi Na.1 (Ubeti wa 27-30, uk. 55).

Uvumilivu katika Ndoa kama Msingi wa Malezi

Waandishi wote wawili wamejadili umuhimu wa wazazi kuvumiliana kama msingi wa ujenzi wa familia bora na malezi ya watoto. Wanawaasa wazazi kuwa wastahamilivu pale kunapokuwa na hitilafu baina yao. Wanapinga tabia ya wazazi kukimbilia kuachana kwa kuwa wathirika wakubwa zaidi ni watoto amba hukosa matunzo ya pande mbili. Badala yake, mwandishi anawaasa wazazi kuwa wamoja

na kushirikiana, kwani malezi yanahitaji ushirika baina ya baba na mama. Haya anayabainisha katika ngonjera ya “Nasaha za Mke” kwa kusema:

Mke: Ujue yako dosari, punguza zako hasira,
 Maisha yetu safari, tuwe na moja dhamira,
 Haufai ujeuri, ule wa mara kwa mara,
 Punguza zako hasira, ujue yako dosari.

Ngonjera: Nasaha na Uzalendo (Ubeti wa 15, Uk. 54).

Katika ubeti huu, mke anajaribu kumuonesha mume umuhimu wa kushirikiana katika malezi ya familia na hasa watoto. Mwandishi anaakisi hali halisi iliyopo katika miji yetu ambapo katika baadhi ya familia suala la ulezzi ameachiwa mwanamke huku wanaume wakiwa hawana habari kabisa. Hivyo, anayalinganisha maisha na safari ndefu, ambapo mume na mke hawana budi kupanga na kusafiri pamoja, tena kwa uangalifu mkubwa na kwa kuvumiliana, ili wafike salama. Hii ni kusema kuwa, kama hawakuwa makini katika safari yao basi abiria (watoto) watawaacha njiani au watapata ajali na kupotea kabisa.

Mwandishi wa *Ngonjera Elimishi Na.1* naye anazungumzia kwa kina umuhimu wa wanandoa kuvumiliana, hasa wanapopita katika vipindi vigumu vya maisha. Kupitia ngonjera ya “Mwanamke Aliyekosa Subira” mwandishi ametanabahisha hatari ya wanawake ambao mapenzi yao yamejengwa katika msingi wa fedha. Anaona kuwa, baadhi ya wanawake hawana mapenzi ya kweli, na wanatishia uhai na ustawi watoto na familia. Zaidi, anaamini kuwa ili watoto wawezi kupata malezi mazuri, ni muhimu kwa wanandoa kuvumiliana, hasa wanapopita katika kipindi kigumu cha maisha. Kupitia ngonjera tajwa mwandishi amemchora mke katika hali ya masononeko makubwa mara baada ya kumkimbia mume aliyekuwa masikini na mgonjwa kitandani; na, baadaye, mwanamke huyo hakuweza kufanikiwa kama alivyodhani. Sehemu ya ngonjera inasema:

Mtangazaji: Hakuwa mwenye subira, upeo wa kungojea,
 Katika yake dhamira, tamaa ilikolea,
 Ndicho chanzo cha hasara, dunia kumwelemea,
 Mambo yakamdodea, kila uchao ugumu

Mtangazaji: Subira jambo muhimu, mtu kuitazamia,
 Huku kazi wajihimu, unajituma kwa nia,
 Ikifika yako zamu, chumo utajichumia,
 Muhimu kuvumilia, subira yavuta heri.

Chanzo: Ngonjera Elimishi Na.1 (Ubeti 54 & 57, Uk. 36).

Katika beti hizi, mwandishi anasisitiza suala la uvumilivu katika ndoa na kупinga tamaa, hasa ya fedha. Mwandishi anaonesha kukerwa na tabia ya wanawake kuwakimbia waume zao pale wanapokosa fedha. Aidha, anaamini kuwa suala la riziki ni siri Mola pekee. Hivyo, anawaasa wanawake kuwa, hawapaswi kubabaika kwa sababu ya fedha au utajiri.

Athari ya Pombe na Dawa za Kulevyta kwa Vijana

Waandishi wa diwani teule wanaona kuwa ulevi na dawa za kulevyta ni majanga ya kidunia na yanahatarisha sana ustawi wa jamii, hasa vijana. Pombe na dawa za kulevyta sio tu zinapunguza nguvu kazi ya taifa bali zinabomoa misingi ya familia. Aidha, huchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la maradhi kama vile kifua kikuu, magonjwa ya ngono na UKIMWI kwa vijana. Vilevile, pombe zinachangia matukio mengi ya hatari kama vile ajali za barabarani na matukio mengine ya uvunjifu wa sheria. Kutokana na hali hii, mwandishi wa *Ngonjera Elimishi Na.1* anaungana na wale wote ambao wamekuwa wakitumia nguvu, mali na akili zao katika kuhakikisha jamii haitumbukii katika hatari hii. Kwa mfano, katika ngonjera ya “Pombe SiiTaki Tena” mwandishi anaonesha hatari ya pombe kwa kusema:

Mke: Watoto wetu wasoma, iliyo mbali skuli,
Na hawafiki mapema, kwani wasomako mbali,
Huwazi wala kusema, uwapatie nauli,
Ili wawahi skuli, kwa kupanda daladala.

Mke: Wewe pesa zako bia, na kuwahonga vimwali,
Ndipo nasisitizia, pombe ina mushkeli,
Lini utajizuulia, kuinywa-lijibu swal?
Ulijibu swal hili, lini pombe utaacha?

Ngonjera Elimishi Na.1 (Ubeti wa 13 & 16, uk. 17-18).

Katika beti hizi mwandishi anajaribu kuonesha hatari ya ulevi na namna inavyorudisha nyuma ustawi wa familia. Anatumia maneno ya mke kuonesha namna ulevi unavyoamaliza fedha za mume na kuongeza ugumu wa maisha katika familia. Vilevile, anaonesha namna ambavyo watu wapo tayari kutumia fedha kwa ajili ya ulevi na kuhonga vimwali (wanawake wa nje) huku watoto wakikosa hata nauli ya kupanda daladala. Zaidi, anaonesha namna ambavyo pombe na uzinzi vilivyo karibu ambapo watu hutumia fedha nyingi kunywa pombe na kuhonga wanawake.

Kwa upande wake, mwandishi wa *Ngonjera: Nasaha na Uzalendo* Vilevile, Nyembe naye anao msimamo kama huu wa kulaani pombe kwa kuwa inaharibu ustawi wa familia. Katika “Nasaha za Mke” mwandishi anasisitiza hili kwa kusema yafuatayo:

Mke: Ni ipi yako huduma, toka kwako siioni,
 Ambazo ni za lazima, asubuhi na jioni,
 Pombe kwako ndio dhima, vingine huvithamini,
 Toka kwako siioni, ni ipi yako huduma?

Ngonjera: Nasaha na Uzalendo (ubeti wa 9, uk. 53).

Katika ubeti huu, mwandishi anaonesha wazi kuwa changamoto mojawapo inayowakabili walevi ni kusahau familia zao. Kupitia sauti ya mke, mwandishi anajaribu kuonesha kilio cha familia kuwa pombe sio mali, na kuwa inachangia kuporomoka kwa malezi ya watoto na familia kwa jumla. Ni wazi kuwa, kalamu ya mwandishi imesawiri hali halisi iliyopo katika miji yetu ambapo wapo wazazi, hasa wa kiume, ambao hawana habari na utunzaji wa familia kutokana na ulevi. Kuhusu madhara ya madawa ya kulevyta, mwandishi ana msimamo ufuatao:

Selemani: Dawa za kulevyta mbaya, jama tuziepukeni,
 Zinakukosesha haya, na kuwa kama shetani,
 Hadhi yako inapwaya, unakuwa mtu duni,
 Tuondoke vijiweni, tuyabadili maisha.

Selemani: Paulo, Issa Rukia, Maiko, Chale na Joni,
 Wamefariki dunia, ulevi ndio kiini,
 Na nyinyi mtaishia, njia hiyo tambueni,
 Haraka jiepusheni, dawa za kulevyta mbaya.

Ngonjera: Nasaha na Uzalendo (Ubei wa 8-9, uk. 23).

Katika kisa hiki mwandishi anamtumia Selemani, ambaye ni kijana, kuwaasa rafiki zake (Joni na Hassani) kuhusu hatari ya uvutaji wa dawa za kulevyta. Mwandishi anayahuishwa madawa ya kulevyta na ugonjwa akili, ukosefu wa haya, kuporomoka kwa hadhi ya mtu katika jamii, pamoja na vifo. Anaonesha wazi kuwa matumizi ya dawa za kulevyta ni hatari kubwa kwa sababu huchangia kupoteza nguvu kazi ya vijana ambayo ni muhimu kwa ustawi wa familia na taifa kwa jumla.

Hitimisho

Ngonjera Elimishi Na.1 na Ngonjera: Nasaha na Uzalendo ni vitabu vizuri vya ngnjera zilizojaa nasaha na mawaidha. Pamoja na maudhui mengine, vitabu hivi vina mawaidha mazuri kuhusu umuhimu wa malezi ya vijana na watoto. Waandishi wanaamini kuwa makundi haya mawili ni muhimu kwa ustawi wa jamii yoyote ile. Vilevile, wanaikumbusha jamii kuwa ustawi wa familia huenda sambamba na malezi imara kwa watoto na vijana. Zaidi, wanaona kuwa jamii yetu inapita katika mawimbi mazito ya kimaadili kwa kuwa familia zimeyumba na hazina wasimamizi na, hivyo, wameamua kutumia kalamu zao kuikumbusha jamii kuhusu malezi ya watoto na vijana.

Marejeleo

- Abdallah, S. (2018). *Nafasi ya Fasihi ya Watoto ya Kidijiti katika Kukuza Fasihi Simulizi: Mifano Kutoka katika Vibonzo Jongevu*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Chikaka, J. K. (2017). *Watoto na Ndoto za Maisha*. Dar es Salaam: DeskTop Production.
- Lyimo, E. B. (2014). “Nduni za Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka katika Vitabu vya Kiswahili ya Fasihi vya Watoto Nchini Tanzania” katika *Mulika* Na. 33. Uk. 33-45.
- Madumulla, J. S. (2001). “Hali ya Vitabu vya Watoto katika Tanzania” katika *Swahili Forum*, Juzu ya 8, uk. 171-183.
- Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.
- Masamba, D. (1983). “Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili” katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*. Dar es Salaam: TUKI
- Mlaga, W. K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.
- Mulokozi, M. M. na Sengo, T. S. Y. (2005). *History of Kiswahili Poetry*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Nyembe, R. M. (2018). *Ngojera: Nasaha na Uzalendo*: Dodoma: Chipanda Printing Inc.
- Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Printing Technology.
- Seif, A. A. (2018). *Ngonjera Elimishi Na.1*. Dodoma: Fex Connect Publishers.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTU.
- Senyamanza, C. E. (2013). *Misingi ya Kazi za Kubuni: Nadharia, Mbinu na Mifano ya Kazi Bunilizi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.